

KAPSABET HIGH SCHOOL

102/2 -

KISWAHILI -

KARATASI YA 2

LUGHA

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

CONFIDENTIAL

Ufahamu

1. AMKENI VIJANA / VIJANA WA LEO / MAISHA NI MAPAMBANO /MAISHA SI MAJAALIWA N.K. (1X1 =1)

2. Maisha yamepangwa na mwenyezi Mungu na binadamu hawezi kubadilisha.

Maisha yana pande mbili nzuri na mbaya na ni lazima uyapitie

Yana utamu na uchungu, raha na dhiki zake (2x1=2)

3.

- ❖ Kushiriki katika migomo
- ❖ Kuvuta sigara
- ❖ Mihandarati / ulevi
- ❖ Ngono
- ❖ Usambazaji wa dawa za kulevya (ulanguzi)
- ❖ Kutotilia elimu maanani
- ❖ Ujambazi
- ❖ Kuwadhulumu wenzao
- ❖ Mavazi ya ajabu / mitindo ya nywele
- ❖ Kuiga wazungu
- ❖ Athari za makundi na rika (peer pressure) (4x1 = 4)

4.

- ❖ Kushiriki ngono ili wapate darahima
- ❖ Kushiriki ulevi
- ❖ Kutembea vilabu na mafuska yenye,ukahaba mwingi (3x1 =3)

5.

- ❖ Vyombo vya habari

- ❖ Kuiga mitindo ya kigeni
- ❖ Ukosefu wa malezi na maadili
- ❖ Ukosefu wa vielezo katika jamii n.k.
- ❖ Vitabu na majarida yenye maelezo na picha chafu
(2x1=2)

6.

- (i) Kufanya msirimbo – usira / mzaha / puuza/ dharau n.k.
- (ii) Unga wa manga si dawa ya chongo – kutenda yasiyofaa huwatumbukiza katika matatizo / kuponda raha sio suluhisho bali ni karaha / kulaumu ugonjwa bila kuchukua tiba si suluhisho (1x3=3)
- (iii) Kwenda mrama / haribika / vurugika nk

2. Ufupisho

(a) Nidhamu

(alama 1)

(b) Umuhimu wa nidhamu:

- Mwenye nidhamu ni nuru nyumbani hata shuleni.
- Anakuwa kiongozi wa wote / watu humtegemea
- watu humpenda.
- Watu humheshimu
- Anajiepusha na shutuma na majanga.
- Kijumla anastahiwa.
- Hupata fursa ya kuteuliwa miongoni mwa wengi kwa dhima fulani.

(Hoja 6X 1 = alama 6, mtiririko al. 1, jumla alama 7)

(c) Muhtasari wa aya nne za mwisho.

- i. Mwadilifu hawezi kuhusishwa na majanga hatari
- ii. Mwadilifu hajipati katika matatizo mengi.
- iii. Utovu wa nidhamu huanzia utotoni
- iv. Mtoto anapozaliwa hutegemea miongozo ya watu wazima walioko karibu
- v. mtoto huiga tabia za wazazi wake na huendelea shuleni.
- vi. Sehemu moja ya ukuaji wa nidhamu ikisambaratika, hawezi kuwa mkamilifu kinidhamu maishani.

- vii. Utovu wa nidhamu hulipwa kwa adhabu mumu humu
viii. watu wajirekebishe kwani uhalifu haulipi

(Hoja $7 \times 1 =$ alama 7, mtiririko al. 1, jumla alama 8)

III MATUMIZI YA LUGHA

- (a) /l/ na /r/ $2 \times \frac{1}{2} = 1$
- (b) (i) Kishazi – kundi la maneno lenye kiima na kiarifu likiwa ndani ya sentensi kuu.
 $1 \times 1 = 1$
- (ii) Nilipompata akilalama ndani ya darasa – kishazi tegemezi
Nilimshauri kupunguza mawazo – kishazi huru $2 \times 1 = 2$
- (c) Mwanafunzi aliyetumwa nyumbani juzi hajapata karo hadi leo. $1 \times 2 = 2/0$
- (d) –enu
k.m. Watoto wenu wana nidhamu $1 \times 2 = 2/0$
- (e) na – kuonyesha mtendaji/kihusishi cha mtendaji
na – ufupisho wa nafsi
- (f) Kula! $1 \times 1 = 1$
- (g) kiwete – A – WA
halmashauri – I-ZI $2 \times 1 = 2$
- (h) Mwanafunzi mtundu hajaiba kitabu kilichonunuliwa jana $1 \times 2 = 2/0$
- (i)

S						
KN			KT			
N	U	N	T	N	V	E
mwalimu	na	mwanafunzi	waliimba	wimbo	mtamu	

- (j) Mshazari ()
- i. Badala ya kiunganishi
 - ii. kutenga tarehe, mwezi na mwaka
 - iii. Kuonyesha maana sawa

Parandisi – [()]

- i. kufungia maneno yatoayo maelezo zaidi kuhusu maneno yanayotangulia
- ii. kuainisha (zingira) nambari au herufi katika orodha
- iii. kutoa maelezo kwa waigizaji

Ritifaa – (‘)

- i. Kuandika sauti za ving’ong’o
- ii. Kuonyesha herufi/nambari iliyoachwa

$$3 \times 1 = 3$$

(k) Jike la jizee hili hupenda matoto sana

$$1 \times 2 = 2/0$$

(l) Thamini – kuchukulia kuwa na hadhi/heshimu/stahi

$$1 \times 2 = 2$$

Dhamini– saidia mtu kifedha kutimiza mahitaji fulani

Musa anathamini elimu hivyo amewadhamini wanafunzi kadhaa shuleni.

(m) Mkurugenzi alisema **kuwa wangelipwa mshahara** wao **siku ambayo ingefuata** na kwamba alikuwa akiendea pesa kwenye benki.

$$6 \times \frac{1}{2} = 3$$

(n) Baba alimnunulia mama gari kwa posho wiki jana (kadiria)

$$4 \times 1 = 4$$

(o) Wa –nafsi (wingi)

Li – wakati (uliopita)

Chimb – mzizi

a – kiishio $(4 \times \frac{1}{2} = 2)$

(p) Viwakilishi nafsi huwa;

mimi – sisi

Wewe – nyinyi huru

Yeye – wao

$$2 \times \frac{1}{2} = 1$$

Nitaingia – tutaingia

Utaingia – mtaingia viambata

Ataingia – wataingia $2 \times \frac{1}{2} = 1$

(q) ogofya

(r) Mama atakuwa amepika tukienda nyumbani (kadiria)

(s) kilimo/zaraa

ISIMU JAMII (ALAMA 10)

a) i. Lafudhi ni upekee wa mtu kuzungumza

ii) Chanzo cha lafudhi

Athari ya lugha ya kwanza

Athari ya lugha nyingine

Kasoro katika ala za matamshi

(zozote 2 x 1 = 2)

b) Sifa za sajili ya matangazo ya soka

i. Lugha changamfu

ii. Lugha legevu

iii. Lugha ya vijalizo(maelezo ya ziada kuhusu mambo yalivyo)

iv. Lugha ya wasifu(sifa za wachezaji na timu zao)

v. Istilahi maalum ya michezo kv bao,nishani,nyota

vi. Kuchanganya ndimi

vii. Msamiati wa kimachachari kv kinyang'anyiro,kizaazaa,kusakata (zozote 7 x 1 = 7)